



# SHIRIKA LA TIJA LA TAIFA

## KOZI YA WASAIDIZI WA OFISI HATUA YA PILI

### Malengo ya Kozi

Kuwaongezea washiriki ujuzi kuhusu taratibu za ofisi utakao wawezesha kuongeza ufanisi mahala pa kazi.

### Walengwa

Wasaidizi wa ofisi, wapokeaji wageni, wapokeaji simu na wale wote waliowahi kuhudhuri kozi ya wasaidizi wa ofisi hatua ya kwanza.

### Mada Muhimu

Utunzaji wa ofisi na mazingira yake; Jinsi ya kushughulikia malalamiko na manung'uniko ya wafanyakazi; Motisha na vivutio kwa wafanyakazi; Nidhamu; Usimamizi wa ofisi; Jinsi ya kuweka na kufikia malengo ya kazi; Mbinu za kuboresha mawasiliano; Vyanzo vya madaraka na usimamizi wa kazi; Kupokea na kutekeleza maagizo; Huduma za masijala; Mbinu za kuboresha huduma kwa wateja; Mahusiano bora kati ya kiongozi na mfanyakazi; Jinsi ya kukabiliana na msongo wa mawazo; Kujenga ushirikiano; Maadili ya kazi; Uandishi wa ripoti; Kuhudumia mikutano; Utunzaji wa siri za ofisi.

### Matarajio

Baada ya mafunzo haya washiriki wanatarajiwa kufahamu taratibu za ofisi

### Mbinu za Mafunzo

Mchanganyiko wa Mafunzo kwa njia ya video, mazoezi kwa vikundi, Uwasilishaji wa mada, mazoezi kwa vitendo.

### Lugha ya Mafunzo

Kiswahili

### Mahali

Morogoro – Kituo cha Tushikamane

### Muda

Wiki tatu

### Tarehe

Kundi	Kuanza	Kumaliza
Moja	11 Novemba, 2019	29 Novemba, 2019
Mbili	11 Mei, 2020	29 Mei, 2020

### Ada na Utaratibu wa Malipo

Ada ni Tshs. **1,110,000/=** na inatakiwa ilipwe kabla ya kuanza kozi kupitia akaunti ya Shirika la Tija la Taifa kwenye Benki ya CRDB, Namba ya Akaunti 01J1042999200, Tawi la Tower; kinyume na hapo mshiriki hataruhusiwa kuhudhuria kozi.

### Jambo la Kuzingatia

Tafadhali zingatia kuwa gharama za safari, chakula na malazi zitagharamiwa na taasisi itakayokudhamini kwenye kozi. Ada yetu imejumlisha gharama za ufundishaji, gharama za utawala, viburudisho vilaini wakati wa asubuhi. Unatakiwa utoe taarifa kwenye ofisi zetu za NIP hapa Dar es Salaam kabla ya kuripoti kwenye mahali pa mafunzo.

### Wasiliana nasi

Nyumba ya Maarifa, Mtaa wa Ohio

S.L.P 2021, Dar es Salaam, Tanzania,

Simu: (+255) 22 2110523/ 2126832/ 2126981 and (+255) 769 291905

Nukushi: (+255) 22 2128619/ 2126081

Barua pepe: [info@niptz.org](mailto:info@niptz.org)

Tovuti: [www.niptz.org](http://www.niptz.org)

